**SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA WAHASIBU, WAKAGUZI NA WASHAURI ELEKEZI WA KODI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**MPANGILIO WA VIFUNGU**


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**KUANZISHWA KWA TAASISI**

3. Kuanzishwa kwa Taasisi.
4. Muhuri na nembo ya Taasisi.
5. Malengo ya Taasisi.
6. Kazi za Taasisi.
7. Uwezo wa Taasisi.

**SEHEMU YA TATU**
**BODI YA WAKURUGENZI**

8. Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.
9. Sifa za Mwenyekiti.
10. Makamu Mwenyekiti.
11. Katibu wa Bodi.
12. Kazi za Bodi.
13. Kamati za Bodi.

14. Muda wa wajumbe wa Bodi.

15. Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

16. Vikao vya Bodi.

17. Akidi ya Bodi.

18. Maamuzi ya Bodi.

19. Taratibu za vikao.

20. Posho la wajumbe.

21. Mjumbe mualikwa.

22. Kubainisha maslahi.

23. Kukasimu kazi za Bodi.


**SEHEMU YA NNE**
**UENDESHAJI WA TAASISI**


24. Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

25. Kazi za Mkurugenzi Mtendaji.

26. Msajili wa Taasisi.

27. Daftari la kumbukumbu.

28. Idara, divisheni na vitengo vya Taasisi.

29. Wafanyakazi wa Taasisi.


**SEHEMU YA TANO**
**LESENI YA KUFANYIA KAZI**


30. Leseni ya kufanyia kazi.

31. Zuio la kufanya kazi kama Mhasibu, Mkaguzi au Mshauri Elekezi wa Kodi.

32. Zuio kwa Mkaguzi na Mshauri Elekezi wa Kodi.

33. Ufanyaji kazi unaokatazwa.

34. Majukumu na wajibu wa Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA

35. Fedha za Taasisi.

36. Bajeti ya Taasisi.

37. Hesabu na ukaguzi.

38. Uwezo wa kuwekeza.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

39. Makosa na adhabu.

40. Adhabu ya jumla.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

41. Utambuzi.

42. Taratibu za usajili.

43. Malalamiko kuhusiana na wanachama wa Taasisi waliosajiliwa.

44. Ada na tozo.

45. Rufaa.

46. Kanuni za Maadili za Kitaaluma.

47. Kufuata viwango.

48. Kanuni.

49. Marekebisho ya Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam.7 ya 2009.

50. Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam.12 ya 2016.

51. Kubakiza.

**SHERIA NAM. 7 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

6/10/................................................, **2022**

# SHERIA YA KUANZISHA TAASISI YA WAHASIBU, WAKAGUZI NA WASHAURI ELEKEZI WA KODI ZANZIBAR NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar, 2022 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Mhasibu" maana yake ni mtu aliyesajiliwa na Taasisi kama Mhasibu wa Umma aliyethibitishwa kufanya kazi za uhasibu;

"Mhasibu Mkuu wa Serikali" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

"Mhasibu Muambata" maana yake ni mhasibu mtaalamu daraja la tatu aliyesajiliwa na Taasisi baada ya kukidhi masharti yaliyowekwa chini ya Sheria hii;

"Ukaguzi" maana yake ni kazi ya kuhakikisha yenye lengo la kupunguza hatari ya kazi ya kuhakikisha katika kiwango kidogo kinachokubalika kwenye mazingira ya kazi husika kama msingi wa maelezo yakinifu ya hitimisho la aliyefanya ukaguzi;

"Mkaguzi" maana yake ni mtu aliyesajiliwa kama Mhasibu Muambata katika kufanya kazi za umma za ukaguzi aliyeidhinishwa kupitia, kuchunguza taarifa za kifedha na kutoa maoni ya ukaguzi chini ya masharti ya Sheria hii;

"Viwango vya Ukaguzi" maana yake ni viwango vilivyotolewa au vilivyokubalika na Taasisi ambavyo mkaguzi aliyesajiliwa atavifuata anapofanya ukaguzi;

"Taasisi inayofanya kazi" maana yake ni taasisi inayotoa huduma za ukaguzi au ushauri elekezi wa kodi chini ya masharti ya Sheria hii;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Kanuni za Maadili za Kitaaluma" maana yake ni Kanuni za Maadili za Kitaaluma zilizoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii au zilizokubaliwa na Taasisi kwa mujibu wa matakwa ya kimataifa;

"Mkurugenzi Mtendaji" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi aliyeteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Mwaka wa Fedha" ina maana kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Taasisi" maana yake ni Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar iliyoanzishwa chini ya masharti ya Sheria hii;

"Mtu aliyepewa Leseni" maana yake ni mtu binafsi au taasisi ambayo imepewa leseni kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

"Mwanachama wa Taasisi" maana yake ni mhasibu, mkaguzi na mshauri elekezi wa kodi akiwa mtu binafsi au taasisi inayofanya kazi iliyosajiliwa;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayeshughulikia masuala ya fedha;

"Msajili" maana yake ni msajili wa wanachama wa Taasisi;

"Taasisi ya kitaaluma iliyosajiliwa" maana yake ni taasisi iliyosajiliwa kisheria chini ya masharti ya Sheria hii kwa ajili ya kutoa huduma za kitaaluma za uhasibu, ukaguzi na ushauri elekezi wa kodi;

"Mshauri Elekezi wa Kodi" maana yake ni mtu binafsi ambaye amesajiliwa na kupewa leseni chini ya masharti ya Sheria hii.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA TAASISI

Kuanzishwa kwa Taasisi.

**3.**-(1) Kunaanzishwa Taasisi itakayojulikana kama Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar.

(2) Taasisi itakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye kurithiwa na muhuri wake, na kwa jina lake kinaweza:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia kwenye mkataba au muamala wowote kwa mujibu wa sheria;

(d) kukopa kiwango chochote cha fedha kutoka katika taasisi yoyote ya fedha kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo ambalo kisheria linaweza kufanywa au kutekelezwa na chombo kinachojitegemea.

Muhuri na nembo ya Taasisi.

**4.**-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Taasisi katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Taasisi katika waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mtendaji au afisa mwengine yeyote wa Taasisi aliyeidhinishwa na yeye.

(3) Waraka wowote unaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Taasisi utawekwa muhuri wa Taasisi na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Malengo ya Taasisi.

**5.** Malengo ya Taasisi yatakuwa ni:

(a) kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa na wanachama wa Taasisi;

(b) kuhakikisha ufikiaji, utunzaji na uendelezaji wa uweledi wa taaluma; na

(c) kushajiisha elimu na viwango vya juu na maadili ya kitaaluma na kuhakikisha panakuwepo na wanachama wa Taasisi walio waadilifu katika sekta za umma na binafsi.

Kazi za Taasisi.

**6.** Taasisi:

(a) itaanzisha na kupitia Kanuni za Maadili za Kitaaluma kwa:

(i) Wahasibu na Wakaguzi Wataalamu ambazo zitaendana na misingi mikuu ya Kanuni za Maadili za Kitaaluma za Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu; na

(ii) Washauri Elekezi wa Kodi;

(b) itahakikisha wanachama wa Taasisi wanalinda viwango vyao vya taaluma;

(c) itahakikisha inatoa huduma bora za kitaaluma kwa wanachama wa Taasisi;

(d) itatoa na kukubali Viwango vya Kifedha na Ukaguzi vya Kimataifa Vinavyokubalika kwa ajili ya kushajiisha matumizi na kufanya mabadiliko sahihi inapohitajika;

(e) itasajili wanachama wa Taasisi;

(f) itachapisha, itaweka na itatunza daftari la kumbukumbu la wanachama wote wa Taasisi;

(g) itadhibiti, itaendesha na itasimamia programu endelevu za elimu za taaluma na itamtaka mtu yeyote aliyesajiliwa chini ya Sheria hii kufuata programu hizo;

(h) itatoa vyeti, leseni na taarifa zinazohitajika kutolewa chini ya Sheria hii;

(i) itaanzisha au itashajiisha tafiti na uchapishaji wa jarida la Taasisi linalohusiana na masomo ya uhasibu, ukaguzi, kodi na mambo mengine yanayohusiana na hayo;

(j) itaweka na kusimamia muundo wa ada zitakazolipwa na wanachama wa Taasisi;

(k) itashajiisha utambulisho wa Taasisi kimataifa;

(l) itasimamia na kuweka utaratibu wa mafunzo yanayoendeshwa na watoa mafunzo ya ziada;

(m) itashajiisha mahusiano baina ya Taasisi na taasisi nyengine zinazohusiana na huduma za uhasibu, ukaguzi na ushauri elekezi wa kodi; na

(n) itafanya kazi nyengine zozote kwa ajili ya utekelezaji wa kazi chini ya Sheria hii.

Uwezo wa Taasisi.

**7.** Katika kutekeleza kazi zake, Taasisi itakuwa na uwezo wa:

(a) kuchunguza au kuhoji yenyewe au kwa kutakiwa na mtu mwengine juu ya lalamiko lolote ambalo limewasilishwa endapo kutakuwa na uvunjaji, kosa, usimamizi mbaya au migongano ambayo imedaiwa, imeripotiwa au imethibitishwa dhidi ya wanachama wa Taasisi;

(b) kuwaita mashahidi, kuitisha vitabu vya hesabu, nyaraka na kuhoji mashahidi na watu wanaohusika;

(c) kupeleleza na kuchunguza kazi zinazofanywa na wanachama wa Taasisi kwa ajili ya kuangalia ubora;

(d) kutaka taarifa yoyote juu ya shughuli zinazohusiana na wanachama wa Taasisi;

(e) kutoa adhabu ikijumuisha kufuta, kusimamisha au kuondoa cheti chochote cha usajili na leseni iliyotolewa chini ya Sheria hii;

(f) kuingia katika makubaliano ya pamoja na vyombo vya kitaaluma vya kitaifa, kikanda na kimataifa;

(g) kuchunguza lalamiko lolote la kimaandishi lililowasilishwa dhidi ya Mwanachama yeyote wa Taasisi, ikiwa Taasisi yenyewe au kutokana na ombi la mtu yeyote; na

(h) kuchukuwa hatua za kinidhamu kutokana na uvunjaji wowote wa Kanuni za Maadili za Kitaaluma.

## SEHEMU YA TATU
## BODI YA WAKURUGENZI

*Uanzishwaji na Muundo wa Bodi.*

**8.**-(1) Kunaanzishwa Bodi itakayojulikana kama Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi.

(2) Bodi itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mhasibu Mkuu wa Serikali;

(c) Mkurugenzi Mtendaji;

(d) Wajumbe watatu kila mmoja kutoka katika Jumuiya ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi; na

(e) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

(3) Isipokuwa Mwenyekiti, Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi Mtendaji, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Taasisi husika kwa kuzingatia mgawanyo wa kijinsia, elimu na uzoefu.

*Sifa za Mwenyekiti.*

**9.** Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti ikiwa mtu huyo:

(a) ana cheti cha Mhasibu wa Umma Aliyethibitishwa au kinacholingana nacho;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika fani inayohusiana; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

*Makamu Mwenyekiti.*

**10.** Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Katibu wa Bodi.

**11.**-(1) Bodi itamteua mfanyakazi mwenye sifa ambaye ni muajiriwa wa Taasisi kuwa Katibu wa Bodi

.

(2) Katibu atawajibika kwa Bodi, na:

(a) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(b) atatunza taarifa sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(c) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe;

(d) atatoa ushauri sahihi kwa Bodi pale unapohitajika; na

(e) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

**12.** Bodi:

(a) itatoa miongozo ya kimkakati kwa Taasisi;

(b) itaajiri wafanyakazi wa Taasisi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;

(c) itaidhinisha:

(i) sifa za usajili;

(ii) usajili wa wanachama wa Taasisi;

(iii) muundo wa ada zitakazolipwa na wanachama wa Taasisi;

(iv) bajeti na taarifa za kifedha za Taasisi;

(v) majina kwa ajili ya utoaji wa vyeti na leseni kwa mujibu wa Sheria hii; na

(vi) mitaala ya masomo na matokeo ya mitihani.

(d) itadhibiti maadili ya kitaaluma ya wanachama wa Taasisi;

(e) itatoa miongozo kwa utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii;

(f) itawashauri wasimamizi wa taasisi za elimu juu ya mitaala ya masomo ya uhasibu, ukaguzi na kodi;

(g) itazishauri taasisi za umma na binafsi juu ya uwajibikaji na usimamiaji wa mambo ya kifedha katika sekta zote za uchumi; na

(h) itafanya kazi nyengine yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Kamati za Bodi.

**13.** Bodi itaanzisha Kamati ya Udhibiti wa Ubora, Kamati ya Mitihani, Kamati ya Nidhamu na kamati nyengine yoyote itakayoonekana inafaa.

Muda wa wajumbe wa Bodi.

**14.** Isipokuwa mjumbe anayeingia kwa nafasi yake, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

**15.** Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi ikiwa mjumbe huyo:

(a) amesitishwa na Waziri;

(b) amejiuzulu au kwa namna yoyote amepoteza sifa ya ujumbe wa Bodi;

(c) ameshindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya ruhusa ya Mwenyekiti;

(d) hawezi kutekeleza kazi za Bodi kwa sababu za kiafya ya kimwili au kiakili;

(e) ametiwa hatiani kwa kosa la jinai linalohusiana na udanganyifu, kutokuwa muaminifu au uvunjaji wa maadili; au

(f) amefariki.

Vikao vya Bodi.

**16.**-(1) Bodi itakutana kikawaida mara moja katika kila miezi mitatu na inaweza kukutana muda wowote kwa vikao vya dharura pale itakapohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zake.

(2) Vikao vyote ya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti na akiwa Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha vikao vya Bodi na ikiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchaguwa mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi ya Bodi.

**17.** Akidi ya vikao vyote vya Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya Wajumbe wake.

Maamuzi ya Bodi.

**18.** Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa maafikiano na ikitokezea hakuna maafikiano, maamuzi yatafanywa kwa kura na ikitokezea kura kuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya maamuzi.

Taratibu za vikao.

**19.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuweka taratibu zake yenyewe kuhusiana na vikao na utekelezaji mzuri wa shughuli zake ikijumuisha Kamati za Bodi.

Posho la wajumbe.

**20.** Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watastahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma na sheria nyengine zinazohusiana.

Mjumbe mualikwa.

**21.** Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi kama mtaalamu lakini mjumbe mualikwa huyo hatakua na haki ya kupiga kura.

Kubainisha maslahi.

**22.**-(1) Mjumbe yeyote wa Bodi ambaye ana maslahi ya kifedha au maslahi mengineyo ya moja kwa moja au vyenginevyo katika kushughulikia jambo husika ambalo liko mbele ya Bodi, atabainisha kwa Bodi uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji uliofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utarikodiwa katika kumbukumbu za kikao hicho.

(3) Mjumbe ambaye atafanya ubainisho chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) hatahudhuria katika majadiliano ya Bodi yanayohusiana na jambo hilo; na

(b) hatashiriki katika maamuzi yoyote ya Bodi yanayohusiana na jambo hilo.

(4) Kwa madhumuni ya kuamua kwamba akidi imetimia, mjumbe aliyejitoa katika kikao au ambaye hakushiriki katika kikao chini ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, atachukuliwa kama kahudhuria kikao.

(5) Mjumbe ambaye atashindwa au atakataa kubainisha maslahi yake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ni mkosa na amevunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Zanzibar.

Kukasimu kazi za Bodi.

**23.**-(1) Bodi inaweza, itakapoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Mkurugenzi Mtendaji, kamati au mfanyakazi mwengine yeyote wa Taasisi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Bodi itatoa maelekezo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelazaji mzuri wa kazi hizo.

## SEHEMU YA NNE
## UENDESHAJI WA TAASISI

Uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji.

**24.**-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji ikiwa mtu huyo:

(a) ana cheti cha Mhasibu wa Umma Aliyethibitishwa au kinacholingana na hicho;

(b) ana uzoefu wa kazi usiopungua miaka saba katika fani ya uhasibu, ukaguzi, kodi au fani nyengine yoyote inayolingana nayo; na

(c) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mkurugenzi Mtendaji.

**25.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu na atatekeleza kazi za kila siku za Taasisi.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mtendaji:

(a) atasimamia fedha, mali na shughuli za Taasisi;

(b) atapanga, atadhibiti na atasimamia wafanyakazi wa Taasisi;

(c) atasimamia na atatekeleza maelekezo yote ya Bodi;

(d) atakuwa mtunzaji wa muhuri, kumbukumbu na nyaraka zote za Taasisi; na

(e) atatekeleza kazi nyengine zozote kwa madhumuni ya utekelezaji wa masharti ya Sheria hii.

Msajili wa Taasisi.

**26.** Mkurugenzi Mtendaji atakuwa ni Msajili wa Taasisi na:

(a) atasajili au atafuta usajili wa wanachama wa Taasisi;

(b) ataweka na kutunza kumbukumbu za wanachama wa Taasisi waliosajiliwa na waliofutiwa usajili;

(c) atatoa cheti cha usajili kwa wanachama wa Taasisi baada ya kuidhinishwa na Bodi; na

(d) atachapisha au atasababisha kuchapishwa, orodha ya wanachama wa Taasisi waliosajiliwa na waliofutiwa usajili ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kila mwisho wa mwaka wa fedha.

Daftari la kumbukumbu.

**27.** Kutakuwa na daftari la kumbukumbu la wanachama wa Taasisi ambalo taarifa zake zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Idara, divisheni na vitengo vya Taasisi.

**28.**-(1) Taasisi inaweza kuanzisha idara, divisheni au vitengo kama itaona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(2) Wakuu wa idara watateuliwa na Bodi kulingana na sifa na uzoefu husika.

(3) Wakuu wa divisheni au vitengo watateuliwa na Mkurugenzi Mtendaji kulingana na sifa na uzoefu husika.

(4) Wakuu wa idara, divisheni na vitengo watawajibika kwa Mkurugenzi Mtendaji.

Wafanyakazi wa Taasisi.

**29.** Taasisi, baada ya kupata idhini ya Bodi na kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, itaajiri wafanyakazi wengine kama itakavyohitajika kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Taasisi.

## SEHEMU YA TANO
## LESENI YA KUFANYIA KAZI

Leseni ya kufanyia kazi.

**30.**-(1) Kutakuwa na leseni ya kufanyia kazi itakayotolewa na Taasisi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, taasisi inayofanya kazi au mtoa mafunzo ya ziada hatofanya kazi mpaka awe na leseni halali ya kufanyia kazi iliyotolewa na Taasisi.

(3) Uhalali wa leseni ya kufanyia kazi utakuwa kwa kipindi cha mwaka mmoja tokea tarehe iliyotolewa na inaweza kuhuishwa baada ya kumaliza muda.

(4) Taratibu za kuomba, kutoa, kuhuisha, kurejesha tena na sababu za kusitisha leseni ya kufanyia kazi zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Zuio la kufanya kazi kama Mhasibu, Mkaguzi au Mshauri Elekezi wa Kodi.

**31.**-(1) Mtu binafsi hatofanya kazi kama Mhasibu, Mkaguzi au Mshauri Elekezi wa Kodi isipokuwa mtu huyo ni:

(a) mshirika au muambata wa taasisi inayofanya kazi iliyosajiliwa; au

(b) muajiriwa katika shughuli za kila siku na amesajiliwa chini ya Sheria hii.

(2) Muajiriwa wa taasisi ya umma anayefanya kazi kama Mhasibu, Mkaguzi au Mshauri Elekezi wa Kodi mtaalamu atatakiwa kusajiliwa.

(3) Mhasibu, Mkaguzi au Mshauri Elekezi wa Kodi mtaalamu wa taasisi ya umma ataruhusiwa kufanya kazi nje ya taasisi ya umma pale atakaporuhusiwa na muajiri wake.

(4) Mtu binafsi hatofanya kazi kama Mshauri Elekezi wa Kodi mpaka awe amejiunga katika taasisi inayofaya kazi iliyosajiliwa.

Zuio kwa Mkaguzi na Mshauri Elekezi wa Kodi.

**32.** Mtu hatoteuliwa au kutoa huduma yoyote kama Mkaguzi au Mshauri Elekezi wa Kodi, mpaka awe na leseni halali ya kufanyia kazi iliyotolewa chini ya Sheria hii.

Ufanyaji kazi una-okatazwa.

**33.** Taasisi inayofanya kazi yenye leseni:

(a) haitomuajiri mtu ambaye amesimamishwa kufanya kazi kama Mhasibu wa Umma Aliyethibitishwa au Mshauri Elekezi wa Kodi kutekeleza kazi zinazohusiana na majukumu yake; au

(b) haitosaini taarifa za kifedha, marejesho ya kodi au waraka mwengine ambao unakusudia kuwakilisha kazi iliyofanywa na taasisi inayofanya kazi mpaka iridhie na ijiandae kuchukuwa jukumu la kazi iliyofanywa.

Majukumu na wajibu wa Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi.

**34.** Majukumu na wajibu wa Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi yataainishwa katika kanuni.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Taasisi.

**35.**-(1) Fedha na rasilimali za Taasisi zitajumuisha:

(a) kiwango cha fedha kama kitakachoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika mfumo wa ruzuku;

(b) fedha zitakazopokelewa na Taasisi kwa ajili ya huduma zilizotolewa na Taasisi;

(c) misaada halali, zawadi, michango, mikopo, urithi au uwekezaji kama Taasisi itakavyoweza kupokea kutoka kwa mtu yeyote au Taasisi; na

(d) fedha nyengine zozote ambazo zitawekwa au kupatikana kihalali na Taasisi, aidha katika kutekeleza kazi zake au vyenginevyo.

(2) Miamala yote ya fedha ya Taasisi itafanywa na kusimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine yoyote ya fedha.

Bajeti ya Taasisi.

**36.**-(1) Mkurugenzi Mtendaji, katika kila mwaka wa fedha, atawasilisha kwa Bodi majadiliano na mapendekezo juu ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi kwa ajili ya Taasisi kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Kutokana na majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Taasisi itafanywa kama ni sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Taasisi yataandaliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na miongozo mengine yoyote inayoweza kutolewa na Serikali kila baada ya muda.

(4) Mkurugenzi Mtendaji atahakikisha kwamba malipo yote yanayotokana na fedha za Taasisi yanafanywa kwa usahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti wa kutosha unafanywa kwa mali na madeni ya Taasisi.

Hesabu na ukaguzi.

**37.**-(1) Taasisi itaweka na kuhifadhi ipasavyo vitabu vya hesabu vya Taasisi.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Taasisi zitakaguliwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimimaizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine za fedha.

Uwezo wa kuwekeza.

**38.** Taasisi itakuwa na uwezo wa kuwekeza fedha zake kwa mujibu sheria husika.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa na adhabu.

**39.** Mtu ambaye:

(a) atapata cheti cha usajili au leseni kwa kutoa taarifa za uongo au udanganyifu wakati wa hatua za maombi;

(b) anafanya kazi ya uhasibu, ukaguzi au ushauri elekezi wa kodi bila ya kusajiliwa au cheti cha usajili au leseni yake imefutwa au imesimamishwa au imeondolewa na Taasisi chini ya Sheria hii;

(c) anafanya kazi ya uhasibu, ukaguzi au ushauri wa kodi bila ya leseni halali;

(d) anatoa cheti chake cha usajili au leseni kutumiwa na mtu mwengine kwa ajili ya kufanya kazi ya uhasibu, ukaguzi au ushauri wa kodi;

(e) anajaribu kutumia au anatumia cheti cha usajili au leseni ya mtu mwengine;

(f) anafanya kazi kama mshauri elekezi wa kodi bila ya kujiunga na taasisi inayofanya kazi; au

(g) anakiuka Kanuni za Maadili za Kitaaluma,

ametenda kosa na, akitiwa hatiani:

(a) ikiwa ni mtu binafsi, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au vyote viwili; na

(b) ikiwa ni taasisi inayofanya kazi, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi au asilimia kumi ya ada ghafi ya ukaguzi, itakayokuwa kubwa, kwa sharti kwamba kiwango kitakachotozwa hakitozidi Shilingi Milioni Thelathini za Kitanzania.

Adhabu ya jumla.

**40.** Mtu ambaye atakiuka masharti yoyote ya Sheria hii ambapo kosa halikuwekewa adhabu maalum, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au kifungo kwa kipindi cha mwaka mmoja au vyote viwili.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Utambuzi.

**41.**-(1) Taasisi itatambua taasisi inayofanya kazi na Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi wote Wataalamu ambao wanafanya kazi Zanzibar kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, namna na taratibu za utambuzi zitaainishwa katika kanuni.

Taratibu za usajili.

**42.** Taratibu za maombi, masharti, makundi ya usajili na mambo mengine yanayohusiana na usajili yataainishwa katika kanuni.

Malalamiko kuhusiana na wanachama wa Taasisi walio-sajiliwa.

**43.** Mtu yeyote anaweza kulalamika kwa Taasisi kwa mwenendo wa Mwanachama wa Taasisi aliyesajiliwa kwa mujibu wa taratibu zilizoanishwa katika kanuni.

Ada na tozo.

**44.** Taasisi itatoza ada na tozo kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Rufaa.

**45.** Mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya Taasisi anaweza kukata rufaa kwa mujibu wa taratibu zilizoainishwa katika kanuni.

Kanuni za Maadili za Kitaaluma.

**46.** Wanachama wa Taasisi watazingatia Kanuni za Maadili za Kitaaluma kama zitakavyoainishwa katika kanuni.

Kufuata viwango.

**47.** Wanachama wa Taasisi watahakikisha ripoti za kazi wanazozifanya au kuziwasilisha zinafuata viwango vilivyoidhinishwa na Taasisi.

Kanuni.

**48.** Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Marekebisho ya Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi,- Nam.7 ya 2009.

**49.** Kifungu cha 62A cha Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam.7 ya 2009 kinarekebishwa kwa:

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kufuta maneno "kwa Kamishna" na badala yake yanawekwa maneno "chini ya Sheria ya Taasisi ya Wahasibu, Wakaguzi na Washauri Elekezi wa Kodi Zanzibar";

(b) kufuta kifungu kidogo cha (2); na

(c) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (3) kuwa kifungu kidogo cha 2.

Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam.12 ya 2016.

**50.** Kifungu cha 19(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Nam. 12 ya 2016 kinafutwa.

Kubakiza.

**51.** Bila ya kujali ufutaji na marekebisho yaliyofanywa chini ya kifungu cha 49 na 50 vya Sheria hii, jambo lolote lililofanywa chini ya vifungu vilivyofutwa au vilivyorekebishwa, litaendelea na litachukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 8 Septemba, 2022.

..............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***